

LEARNING BY EAR

“The Lost Kid – the Story of Single Mothers in Africa”

EPISODE 2: “Looking for Begidu”

AUTHOR: Mantegaftot Sileshi Siyoum

EDITOR: Stefanie Duckstein, Adrian Kriesch

PROOFREADER: Kate Hairsine

List of characters by scene:

SCENE ONE: MORNING AT ASKALE’S HOUSE

- Askale (f, 21)
- Kassech (f, 22)
- Narrator (m, around 35)

SCENE TWO: MORNING AT BELETU’S HOUSE

- Papa Telahun (m, 76)
- Mama Beletu (f, 65)
- Drunkard Minabu (m, 55)
- Narrator (m, around 35)

SCENE THREE: MORNING IN THE SUBURB

- Chala (m, 17)
- Mekete (m, 16)
- Jonas (m, 15)
- Narrator (m, around 35)

SCENE FOUR: MID NIGHT AT BELETU’S HOUSE

- **Papa Telahun (m, 76)**
- **Mama Beletu (f, 65)**
- **Kassech (f, 22)**
- **Narrator (m, around 35)**

INTRO:

Hamjambo! Hiki ni kipindi chetu kipya cha mchezo wa redio cha mfululizo wa Noa Bongo Jenga Maisha Yako kiitwacho “MWANA MPOTEVU-KISA CHA KINA MAMA WANAOWALEA WATOTO WAO BILA BABA ZAO BARANI AFRIKA”. Kwenye sehemu iliyopita, Kassech aligombana na nduguye mdogo Jonas kwa kuwa alikuwa ameondoka nyumbani usiku wa manane. Aliporudi chumbani mwake alipiga kelele kwa hofu. Kwa nini lakini? Hayo utayajua katika sehemu yetu ya pili ya “KUMTAFUTA BEGIDU”. Tuwasikilize kina mama hawa wachanga Kassech na rafiki yake, Askale. Ni asubuhi na akina mama hao wawili wanajiandaa kunywa chai nyumbani kwa Askale.

SCENE ONE: MORNING AT ASKALE’S HOUSE

1. SFX: MORNING AMBIENCE FROM OUTSIDE

2. SFX: TEA BOILING

3. Kassech: (Cries) Mwanangu ametoweka, Askale, mwanangu wa pekee ametoweka! Oh! Nitakuwa mgeni wa nani mimi!

4. Askale: Keti, Kassech, tafadhali.

5. SFX: PULLING A CHAIR

6. Kassech: (Cries) Nilipoamka jana usiku, mlango wa chumba changu ulikuwa wazi!

- 7. Askale:** Usiku?!
- 8. Kassech:** Usiku wa manane!
- 9. Askale:** Nani aliyefanya hivyo, ni mwizi?
- 10. SFX:** **POURING TEA IN THE CUP**
- 11. Kassech:** La, ni ndugu yangu!
- 12. Askale:** Jonas?
- 13. Kassech:** Naam.
- 14. Askale:** Mbona?
- 15. Kassech:** Sijui, Askale. Aliufungua mlango kisha akatoka nje. Nilimfuata lakini akakataa kurudi ndani!
- 16. Askale:** Ajabu! (**She sips the tea**) Kwa nini?
- 17. Kassech:** Alijifanya kwamba alikuwa akiota akitembea lakini nadhani alikuwa na njama fulani. Ebu niambie, kwa mimi siwatunzi vizuri ndugu yangu Jonas pamoja na mwanangu Begidu?

- 18. Askale:** Hapana, Si kweli hata kidogo, Kassech. Mwanao Begidu yuko salama. Usiwe na wasiwasi. Hakutoweka jana kwa kweli. Alilala nyumbani kwa Papa Tilahun.
- 19. Kassech:** Oh, Mngu ni mkubwa. Acha niende nikamuone.
- 20. Askale:** Ebu tulia! Najua unataka kuwa mama mwema kwa mwanao lakini huna budi kumtunza vyema. Anahitaji mapenzi yako!
- 21. Kassech:** Una maana gani?
- 22. Askale:** Mwanangu Samy aliniambia mara kwa mara Begidu humuomba ampe mkate au matunda.
- 23. Kassech:** Wasema nini?! Yaani wanitaka kukaa kusikiliza mambo hayo? Asante sana mwenzangu. Nina mengineyo ya kushughulikia. **(she stands up)**.
- 24. SFX:** **PULLING A CHAIR**
- 25. Askale:** Subiri, Kassech! Mbona huwa uko mbioni kila mara tunapotaka kuzungumzia mwanao?
- 26. Kassech:** Unataka kuniambia nini kuhusu mtoto wangu?
- 27. Askale:** Najua sisi sote ni masikini, lakini bado tuna mengi ya kuwapa watoto wetu.

28. Kassech: Kwani unafikiri simpendi mwanangu?

29. Askale: Hapana, sisemi hivyo. Mwenyewe wajua kwamba ingawa Samy ni mdogo wa Begidu kwa mwaka mmoja, anamshinda hisabati, anajuwa vyema abjadi (alfabeti) na anweza kujielezea vyema.

30. Kassech: **(Angrily)** Asante!

31. Askale: Ninamshughulikia kwa wingi. Ninamsaidia kufanya kazi za shule, ninacheza naye mchezo apendao zaidi. Huwa akiniambia wakati anapotatizwa na jambo au anapofurahishwa na jambo alilolitenda.

32. Kassech: **(Sarcastically)** Haya, hongera kwa mwanao mwerevu na mwenye adabu!

33. SFX: WALKING TO THE DOOR

34. SFX: SLAMS THE DOOR

35. ASKALE: (SIPS THE TEA)

36. NARRATOR:

Askale anakunywa chai yake huku akifikiria tabia ya rafiki yake.

Alitaka kumuuliza Kassech kilichomsababisha kuacha masomo ya

jioni, lakini Kassech akatoka chumbani mwake kabla hajamgusia
suala hilo.

SCENE TWO: MORNING AT BELETU’S HOUSE

37. **SFX:** **MORNING AMBIENCE**
38. **SFX:** **DOOR KNOCKING**
39. **Papa Tilahun** **(Prays in a low voice).**
40. **Mama Beletu:** Karibu, Mlango u wazi.
41. **Papa Tilahun:** **(Still praying in a low voice)** Mwenzetu nani?
42. **Mama Beletu:** Unaswali ama umekaa kuchungulia mlango?
43. **Papa Tilahun:** **(Prays in a low voice).**
44. **SFX:** **DOOR OPENING**
45. **Mama Beletu:** Oh! Minabu, ni wewe. Njoo huku.
46. **Minabu:** **(In a low voice)** Habari za asubuhi, Mama Beletu!
47. **Mama Beletu:** Nzuri!
48. **Minabu:** **(whispers)** Alaa, Papa Tilahun anaswali.

Nitakuja baadaye.

49. **Papa Tilahun:** La, la, subiri! Nimeshamaliza.
50. **Mama Beletu:** Lakini umeanza kuswali hivi punde!
51. **Papa Tilahun:** Ni sawa, Nitakamilisha swala zangu baadaye.
52. **Minabu:** **(In a polite manner)** Shikamoo, mzee!
53. **Papa Tilahun:** He, he, he! Si wewe hapo! Mchana utandani malaika lakini usiku ukirudi hata Ibilisi afadhali!
54. **Minabu:** Nimekuja kukuomba msamaha, Papa Tilahun.
55. **Papa Tilahun:** Sikiza vizuri! Minabu,ukiendelea kuwasumbua majirani zako kila usiku, nitakutimua! Wala si utani!
56. **Minabu:** Ninatoa ahadi, nitaacha!
57. **Papa Tilahun:** Haya, ila kumbuka ni rahisi kutoa ya kuacha usumbufu. Ngoma itakuwa usumbufu wa kutafuta nyumba nyingine ya kupanga. Nishakuambia niliyokuwa nayo! **(Minabu leaves).**
58. **SFX:** **DOOR OPENS AND CLOSES**

59. Mama Beletu: Minabu ni mtu aliyesoma; usimtendee kama mtoto mdogo.

60. Papa Tilahun: Sioni tofauti yoyote ikiwa kazi yake ni kulewa na kuwasumbua majirani. **(Prays in a low voice).**

61. Mama Beletu: Lakini...

62. Papa Tilahun: Hakuna cha lakini! Niache nimalize dua zangu. **(Prays in a low voice).**

63. NARRATOR:

Mambo kawaida kama sheria. Minabu hulewa usiku akawatatiza majirani; kisha siku inayofuata jogoo la kwanza anamwendea mwenye nyumba Papa Tilahun kumuomba msamaha na kutoa ahadi asizozitimiza.

Sasa, tujishughulishe na vijana wawili, ambao mlevi wetu Minabu aliwaona jana usiku gizani. Ni Makete, mwenye umri wa miaka kumi na sita na rafiki yake Challa mwenye umri wa miaka 17. Jonas, ndugu mdogo wa Kassech yuko pamoja na vijana hao wawili.

SCENE THREE: MORNING IN THE SUBURB

64. **SFX:** **MORNING AMBIENCES**
65. **SFX:** **DOG BARKS**
66. **Jonas** Ama mumlishe huyo mbwa kipande cha mkate au mumpe sumu!
67. **Challa:** Wewe! Bobbie, nenda zako! **(Throws a stone and hits the dog).**
68. **SFX:** **DOG WHINES AND RUNS AWAY**
69. **Challa:** Hatuwezi kupanga jambo lolote wakati huyo mbwa mpumbavu akiwepo!
70. **Mekete:** Jana usiku, nusura yule mlevi atutambuwe!
71. **Challa:** Kisa na maana ni huyu mbwa mwenye njaa!
72. **Jonas:** Si hoja tunayosema, mpango wetu ulitibuka.
73. **Challa:** **(Laughs)** Hata hivyo nilifurahia jana usiku jinsi ulivyojifanya kwamba ulikuwa ndotoni. Uliigiza vizuri mara tu mpwa wako alipogunduwa mlango ulikuwa wazi.

74. Mekete: **(Laughs)** Naam, ulitenda mambo sawa! Na sasa una uhuru kutoka nyumbani kwa dadako. Unaweza kukaa hapa kwetu kwa muda wowote unaotaka; nishazungumza na babangu akuruhusu ukae kwetu.

75. Jonas: Sawa, jana hatukuweza kuingia nyumba ya Papa Tilahun. Nadhani tunapaswa kutafuta mtu mwingine tajiri anayeishi katika kitongoji chetu.

KW begin

76. Challa: Naam! Nakubaliana nawe!

77. Mekete: Safi!

78. SFX: **DOG APPROACHES, BARKING**

79. Challa. Balaa! Huyu tena mbwa msumbufu... **(Throws a stone and hits the dog again).**

80. SFX: **DOG WHINES AND RUNS AWAY**

KW end

81. Narration: Vijana hao watatu wameamua kuwa mara ijayo watajaribu kuvunja nyumba ya Bwana Kasu ambaye ni tajiri wa kupigiwa mfano. Wakati huo huo, Kassech anaelekea nyumbani kwa Mama Beletu na Papa Tilahun, kumtafuta mwanawe aliyetoweka.

SCENE FOUR: AT BELETU’S HOUSE

82. SFX: MORNING AMBIENCES

83. Papa Tilahun: Sikiza, Kassech, ikiwa unataka kusalia kuwa mpangaji hapa, hii tabia lazima uikomeshe mara moja!

84. Mama Beletu: Nimeshamwambia ulipokuwa ukiswali. Anasikitika sasa kwa tabia yake hiyo.

85. Kassech: Nawaomba nyote wawili mnisamehe. **(cries)**. Mambo yalinizidia jana.

86. Mama Beletu: Usilie, mwanangu, umeshaniambia kila kitu.

87. Papa Tilahun: Si hoja aliyokwambia, katu sitaruhusu tena majirani kusumbuliwa! Fauka ya hayo, unapaswa kumtunza vyema mwanao! Kama mjukuu wetu wa kike asingempata mwanao, Bedigu, jikoni jana usiku, mambo sijui yangukuwa vipi?

88. Kassech: **(sobs then cries)** Nafanya kazi kwa bidii kila siku kutafita chakula cha kutulisha sisi watatu, na pia ninataka kutundiza fedha ili nipate kurejea kwenye masomo ya jioni.

- 89. Papa Tilahun:** Bila shaka, mwanangu, tunajua vyema kwamba unafanya kazi kwa bidii!
- 90. Kassech:** Ninamtunza Begidu, ninahakikisha kwamba ana chakula cha kutosha. Lakini hapaswi kutaka vitu ambavyo sina uwezo wa kumpa! Mimi niliyapitia maisha yayo hayo!
- 91. Papa Tilahun:** Unaona, hilo ndilo tatizo!
- 92. Mama Beletu:** Ndiyo, sisi pia tuliyapitia maisha hayo. Hata hivyo hatupaswi kuwatendea watoto wetu jinsi tulivyotendewa hasa ikiwa tunaweza kuwatendea vyema zaidi.
- 93. Papa Tilahun:** Kweli! Hatupaswi kufanya hivyo! Mama Beletu, hukumbuki vile mtoto wetu alivyotuambia mara ya mwisho tulipokuwa likizoni Ulaya? Alitweleza umuhimu wa wazazi kuwalea watoto wao kwa njia njema.
- 94. Mama Beletu:** Nayakumbuka yote aliyoyasema!

KW BEGIN

Alitueleza habari ya shule zao za chekechea na jinsi walimu wa chekechea wanavyowatia shime watoto. Karibu watoto wote huko huhudhuria shule za chekechea.

95. **Papa Tilahun:** Genau! (**laughs**)
96. **Mama Beletu:** Naam, mtoto wetu alituambia neno hilo
“genau” la kijerumani lina maana ya “kweli”.
97. **Papa Tilahun:** Hakika.
98. **Mama Beletu:** Vizuri,
99. **Papa Tilahun:** Swadakta,
100. **Mama Beletu:** Na sawasawa!
101. **Papa Tilahun:** Kwa hivyo, Kazi ya ulezi wa mtoto wako
haitegemei umasikini au utajiri wako,
inalingana na jinsi unavyotumia bongo lako.
102. **Mama Beletu:** Genau! (**Both laugh**).

KW END

103. **Papa Tilahun:** Endapo unanua kumlea mwanao akiwa na
nguvu na furaha, unapaswa kutumia muda
mwengine ukiwa naye. Baadhi ya njia za
kumkuza mwanao kiakili tangu akiwa mdogo ni
kujibu maswali yote anayouliza bila kuchushwa
naye, kumhadithia hadithi na kusaidia kufanya
kazi za shule.

104. Mama Beletu: Tukiwatelekeza watoto wetu hii leo, hatimaye wataitaliza jamii kwa kiasi kikubwa.

105. Papa Tilahun: Hivyo ndivyo tulivyofunzwa na mwanetu. Wajua, Begidu anaonekana kuwa na wasiwasi zaidi ya wenzake. Hii ni dalili kwamba mtoto hajiamini. Unaweza kumfanya ajiamini kwa kumpa mapenzi zaidi!

106. Kassech: Sawa! Sasa unaweza kumchukua twende nyumbani?

107. Papa Tilahun: Naam! Anacheza pamoja na Aster mjukuu wetu katika chumba cha pili.

108. Mama Beletu: **(Walks to the next room and calls)** Aster!
Aster! Aster!

OUTRO:

Na hapa tunahitimisha sehemu ya pili ya kipindi chetu cha mchezo wa redio wa Noa Bongo Jenga Maisha Yako kiitwacho “ **Mwana Mpotevu- Kisa cha kina mama wawaleao watoto wao bila baba zao barani Afrika**”. Baada ya kupawa ushauri na watu hawa wawili wenye busara, je Kassecha atatenga muda zaidi wa kuwa na mwanawe? Na je vijana hao watatu wana njama gani? Kwa taarifa zaidi, jiunge nasi kwenye sehemu itakayofuata. Kumbuka iwapo unataka kusikiliza kipindi hiki tena, au kuwasilisha maoni na mapendekezo yako, fungua ukurasa wa tovuti dw.de/lbe. Kwaheri kwa

sasa!